**LEARNING BY EAR - "Girls' Rights"**

**EPISODE 10**

**Title: "Careers for Girls" – A Story of Girls' Rights**

**AUTHOR**: **Njoki Muhoho**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Michael Lawton**

**Kisuaheli:Eric Ponda**

**Characters:**

**SCENE 1 CLASSROOM**

Narrator - 30s Male
Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Fatuma - 14 Female
Abdi - 15 Male

**SCENE 2 - TEACHER MONA CLASS**

Teacher Mona - 35 Female
Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Fatuma - 14 Female
Abdi - 15 Male
Crowd of boys and girls in the classroom

**SCENE 3 - TEACHER MONA CLASS**

Narrator - 30s Male
Teacher Mona - 35 Female
Ciro - 14 Female
Cheptoo - 15 Female
Abdi - 15 Male
Crowd of boys and girls in the Classroom (14-16)

**01. <u>INTRO</u>**

**02. <u>MUSIC: THEME MUSIC</u>**

03. **NARRATOR** Hujambo na karibu kwa makala nyingine ya Learning By Ear, Noa Bongo jenga Maisha yako katika kipindi cha kumi na cha mwisho kwenye mfululizo wa mchezo huu kuhusu **Haki za Wasichana.**Katika vipindi vyote tisa vilivyotangulia kwenye mchezo huu,Ciro, Cheptoo na Fatuma wanakumbwa na changamoto mbali mbali ambazo wamekuwa wakizijadilia katika bunge leo la wasichana. Hivyo basi ungana na wasichana hawa katika safari yao ya mwisho wanapojadilia hoja kuhusu **Kuchagua taaluma.**

**<u>SCENE 1: CHEPTOO'S CLASSROOM</u>**

**04. <u>SFX: DOOR OPENS</u>**

05. **CIRO** Cheptoo,, unafanya nini darasani wakati huu wa mapumziko?. Tumekusubiri kwa muda mrefu sana kule uwanjani.

06. **FATUMA** Ssssh, Ciro, pole pole …anasoma.

| | | |
|---|---|---|
| 07. | **CIRO** | Cheptoo unasoma … wewe? Ha ha<br><br>(STARTS SINGING) Cheptoo anasoma, Siku hizi amekuwa ***siridado****…yaani* mpezni wa vitabu… |
| 08. | **CHEPTOO** | (AGITATED) Ciro, Fatuma! Hebu niondokeeni hapa! Hamuoni nina shughuli nafanya. |
| 09. | **CIRO** | Nimeanza kuwa na shaka!. Si yule ni binamu yangu pale pembeni? Yule pale nyuma ya Dawati? (LOUDLY) Abdi pia wewe unasoma wakati huu wa kupumzika. Sawa! Ni jambo la kushangaza sana! Hivi…,si nyinyi wawili mlikuwa watu wa kwanza kutoka darasani wakati wa mapumziko baada ya masomo au kwa chakula cha mchana. |
| 10. | **CHEPTOO** | Basi kwa taarifa yenu mnapasa kujaza hizi hizi za kuchagua taaluma. |
| 11. | **CIRO** | (STARTS SINGING AGAIN) “Mchangamkia kazi”…. ndio taaluma ya Cheptoo!. Cheptoo, Cheptoo ni siridado ziku hizi. |

| | | |
|---|---|---|
| 12. | **ABDI** | Nyamaza Ciro! Hili ni jambo la muhimu sana! Mona uwatatize?. |
| 13. | **FATUMA** | Kwani kuna ugumu gani wa kuchagua taaluma? Cheptoo, unataka kuwa nini maishani.? |
| 14. | **CHEPTOO** | Mtaalam wa Biokemia! |
| 15. | **CIRO, FATUMA,ABDI** | CRUDE LAUGHTER |
| 16. | **ABDI** | Nini? Kwani hata una habari mtaalam wa Bio Kemia anafanya nini? |
| 17. | **CHEPTOO** | (INTERRUPTS QUICKLY) Mtaalam wa Bio Kemia ni mwanasayansi aliyesomea masuala ya Biokemia. Na Bio Kemia ni elimu kuhusu mabadiliko na jinsi kemikali zinavyofanya kazi katika viumbe…. |
| 18. | **CIRO** | (JUBILATING) Wow, kongole msichana…,msimamo ni huo huol. |
| 19. | **ABDI** | Sawa,..wewe ni msichana! |
| 20. | **CHEPTOO/CIRO** | Kwa hivyo? |
| 21. | **ABDI** | Kuna taaluma za wanaume na taluma za wanawake.Na huo ndio ukweli wa mambo. |

22. **FATUMA** Hizo ni sheria za Abdi au vipi? Hata hivyo lakini ni sawa. Hebu twambia bsi taaluma yako ni gani?

23. **ABDI** Kuna taaluma kadhaa. Bado sijaamua lakini!.

24. **CHEPTOO** (IRRITATED) Bado hujaamua..! ndiyo taaluma gani hiyo, Abdi?.

**SCENE 2: TEACHER MONA'S CLASS**

**25. SFX: BELL RINGS**

**26. SFX: STEPS INTO THE ROOM. FURNITURE MOVEMENT NOISES. SOUNDS: STUDENTS MURMURING (partly studio)**

27. **TEACHER MONA** Habari ya asubuhi wanafunzi. Ketini

28. **CLASS** Ni nzuri Mwalimu Mona.

29. **TEACHER MONA** Fatuma na Ciro, mnafanya nini katika darasa hili, mnapasa kuwa katika darasa lenu. Nendeni sasa kabla ya kujipata mashakani.. Waalimu wenu. .

| | | |
|---|---|---|
| 30. | **CIRO** | Mwalimu Mona, hapa tunatatizo la kuchagua taaluma. Abdi anasema Cheptoo hawezi kuwa mtaalam wa masuala ya Bio Kemia eti kwa sababu ni msichana!. |
| 31. | **TEACHER MONA** | Kumbe kuna tatizo hapa. Sasa wanafunzi wengine mwasemaje?. Je kuna kazi za wasichana na wavulana? |
| 32. | **CLASS** | Ndiooo.. hapana… ndiooo! |
| 33. | **CHEPTOO** | Mwalimu bora tuitishe kikao cha bunge la wasichana kujadilia hoja hii!' |
| 34. | **TEACHER MONA** | Sawa basi, wasilisheni Hoja hiyo. |
| 35. | **CHEPTOO** | Napendekeza hoja kwamba hakuna kazi za wavulana ambazo haziwezi kufanywa na wasichana!.' |
| 36. | **ABDI** | Napinga hoja hiyo.Kuna baadhi ya taaluma zinafaa kufanywa na wavulana pekee na wala sio wasichana! |
| 37. | **CIRO** | Abdi, wewe una mzaha sana…una… |
| 38. | **TEACHER MONA** | Order, order… Ciro, huu ni mjadala |

| | | |
|---|---|---|
| 39. | **CHEPTOO** | Nasimama kwa hoja ya nidhamu kwamba wasichana wanauwezo sawa na wavulana katika taaluma zote. Msingi ni uwezo wa kutekeleza taaluma hiyo wala sio tofauti ya kijinsia. |
| 40. | **ABDI** | Umekosea. Jukumu la wanawake ni malezi majumbani. Taaluma zao zinapasa kuwa zile zinazofungamana namasuala ya malezi kama vile wauguzi, Waalimu na washauri na sivinginevyo... |
| 41. | **CIRO** | (INTERRUPTS) Jinsi unavyoongea huna tofauti na Mababu zetu wa karne zilizopita. Msichana anaweza kuwa mhandisi. |
| 42. | **ABDI** | Lakini hiyo lazima ufanye vyema katika mtihani wako hasa katika somo la Fizikia na Hesabu. Na wasichana hawayawezi Masomo haya. |
| 43. | **CIRO** | Wewe na wengine wenye fikra sawa na zako mnataka tuamini hivyo sivyo. Basi mmekosea. |
| 44. | **FATUMA** | Abdi, Mimi hufanya vyema zaidi hasa katika masomo haya. |

| | | |
|---|---|---|
| 45. | **ABDI** | Sasa kuna haja gani kama wazazi wako wanataka uolewe hata kabla ya kukamilisha masomo yako! Huwezi kuwa mhandisi. |
| 46. | **FATUMA** | Nitakuwa mhandisi. |
| 47. | **ABDI** | Wasichana hawataki kufanya kazi za nje.Hawataki kuchafuka. Na shangazwa na Cheptoo mwenye kupenda urembo wa mavazi ya kisasa, na kurembesha kucha zake kwamba ni vipi ataweza kufanya kazi kama mhandisi. Hebu fikiria wewe.. na.na Cheptoo katika Ovaroli, katika kazi ya kujenga barabara na daraja? |
| 48. | **CHEPTOO** | (ANGRY) Abdi, unaniudhi sana.Unaubaguzi wa kijinsia.…wewe.. |
| 49. | **TEACHER MONA** | Order, Order… Punguza hasira. Ni muhimu kulijadilia kwa kina na kupata maoni ya kila mmoja. Twendelee. Abdi? |
| 50. | **ABDI** | Wasichana wanapokuwa watu wazima, wanaolewa, na kisha jukumu lao linakuwa lile la malezi ya Watoto na waume zao. Huwa ni tatizo kwao kufanya kazi za mbali au za usiku. |

| | | |
|---|---|---|
| 51. | **FATUMA** | Abdi,bado unaishi katika enzi za kale wakati wanaume walikuwa wawindaji na kuwaacha wake zao kulea familia wanapokuwa wawindoni. Yaani huoni mambo yamebadilika, ambapo sasa siku hizi wanawake wanafanya kazi za kila aina? |

52. **SFX: (STOMPING OF FEET), CLAPPING HANDS** (studio)

| | | |
|---|---|---|
| 53. | **GIRLS** | Mwambie… mwambie… mwambie |
| 54. | **ABDI** | Lakini ..nyinyi …wasichana.. |
| 55. | **CIRO** | (INTERRUPTS) Lakini nini, hee wasichana wananini Abdi? Tazama ndani ya  darasa hili, wasichana ni wengi kuliko wavulana, kwani iwe tifauti katika kuchagua  taluma? |

**56. SFX: (STOMPING OF FEET), CLAPPING HANDS**

| | | |
|---|---|---|
| 57. | **GIRLS** | Mwambie …mwambie.. Mwambie… |
| 58. | **CHEPTOO** | Isitoshe  siku hizi mtu anaweza kujipanga masaa ya kufanya kazi. |
| 59. | **ABDI** | Lakini kuna baadhi ya taaluma ambazo ni ngumu kwa wasichana. Nadhani utakubaliana nami. |

60. **CHEPTOO** (ANGRY) Tunataka wavulana watuorodheshee taaluma zote na sababu kwanini wasichana hawawezi kuzifanya.

61. **TEACHER MONA** Wazo zuri sana. Sasa tujipange makundi kuorodhesha taaluma hizo. Kisha tutasikia kwanini wasichana hawawezi kufanya taaluma hizo, isipokuwa wavulana pekee.Endeleeni kujadiliana.

**62. ALL: LOUD AND ACTIVE MURMURINGS OF GIRLS AND BOYS**

**SCENE 3: CLASSROOM**

**63. ALL:** HEATED MURMURINGS

64. **TEACHER MONA** Order, Order, Order

65. **ALL:** MURMURINGS CONTINUE

66. **TEACHER MONA** (LOUDLY) Order!!!

**SILENCE**

| | | |
|---|---|---|
| 67. | **TEACHER MONA** | Sasa kutoka upande wa wavulana namualika Abdi kutoa maoni  Ni taaluma gani ambazo ni changamoto kubwa kwa wasichana, na ni zipi wasichana wanaogopa kuzifanya. Pia nanyi wasichana mjiandae kutoa sababu zenu. Na Cheptoo,tafadhali utawakilisha upande wa wasichana. Usichukua muda mwingi tafadhali. |
| 68. | **ABDI** | (CLEARS THOUGHT) Wasichana wanakumbwa na changamoto nyingi katika kufuatilia taaluma zinazohusiana na somo la hesabu.Kwasababu hawawezi sana  somo la hesabu. |
| 69. | **CHEPTOO** | Kwanini basi wanawake  hufanya vyema zaidi katika usimamizi wa fedha nyumbani.?Kwani hiyo haihitaji hesabu. Watu wanasema kuwa wasichana hawawezi somo la hesabu. Tunaweza na tutaweza!. |
| 70. | **ABDI** | Wanawake pia hawapendi kufanya kazi usiku. Hata hivyo nin hatari sana kwao kufanya kazi za usiku. Hawezi kazi mfano kazi za Hotelini, viwanja vya ndege na kadhalika.… |

| | | |
|---|---|---|
| 71. | **CHEPTOO** | Wavulana zindukeni hii ni karne ya 21.Ofisi pia hufanya kazi kwa masaa mengi zaidi hadi nyakati za usiku na Watu hufanya kazi kwa zamu.Tayari mifano hii inadhihirisha kwamba si kweli asemavyo.Wauguzi wengi na madaktari wa kike hufanya kazi usiku Hospitalini.Mimi naamini kwamba ni wavulana wanaoendeleza uongo huu kama njia ya kutuogofya.wanaotogofya kufanya kazi hizi za usiku. Kama kweli wanahofia usalama wetu kufanya kazi za usiku, basi watupe ulinzi! |
| 72. | **GIRLS** | Wambie ..wambie.. wambie.…. |
| 73. | **CIRO** | (SOTTO TONE)Wanafanya kila juhudi kutuogofya.Inakuwaje tumo hatarini mbele ya wanaume na sio wanawake!! Ninyi ni kama nduma kwili. |
| 74. | **GIRLS** | (LOUD SHOUTING) Wambie.. wambie wambie… |
| 75. | **TEACHER MONA** | Order, order. Endelea Abdi. |

76. **ABDI** Wasichana si wajasiri kufanya michezo ya hatari kama vile kushiriki katika mashindano ya mbio za magari.masumbwi,na kukwea milima.Hamuwezi kuwa wanajeshi , na nahakika mtasitasita kufyatua risasi wakati mnapo pelekwa vitani…wewe…

77. **CHEPTOO** Hizo ni dhana zako Abdi!. Kila mmoja anaweza kushiriki mchezo wowote aupendao. Na pia wanawake wanaweza kuwa wanajeshi.Kwani unataka kusema wanawake hawashiriki michezo ya Olimpiki? Unamaanisha wanawake wanaweza kustahamili uchungu wa kujifungua lakini sio kushiriki michezo. Fungua macho, Abdi, usiwe mjinga.

78. **TEACHER MONA** Order..Order… Cheptoo.. punguza hasira….

79. **CHEPTOO** (CONTINUES)…. Abdi…usinifanye nikasirike.. wewe… wewe..

80. **TEACHER MONA** **Tosha**!! Tosha ..Cheptoo, Abdi, tuko hapa kujifunza. Tuko hapa kujaribu kuelimishana kushawishiana kwamba kila mmoja yuko huru kuchagua taaluma aipendayo . Tunataka wavulana watueleze na kutupa sababu kwanini hatuwezi.. kutupa muongozo, na tunasubiri kuelimisha kuhusu hayo,…kwani tupende tusipende hizi ndizo changamoto tunazokumbana nazo sisi wanawake kila siku.Kwa tunamshukuru kila mmoja wenu kwa kushiriki mjadala huu kwa uwazi kabisa.

**81. SFX: LOUD AGREEMENT**

| | | |
|---|---|---|
| 82. | **TEACHER MONA** | Ciro,Unaweza kufunga mjadala huu. |
| 83. | **CIRO** | Ni nawazo zuri zaidi Mwalimu! Tunawashukuru wavulana kwa kufungua macho kuhusiana na tatizo kubwa linalotukumba inapofika suala la wasichana kuchagua taaluma. Na kumalizia,Mwalimu Mona tuna wimbo tunaotaka kuimba. |
| 84. | **TEACHER MONA** | Haya imbeni? |
| 85. | **CIRO** | Wimbo wenyewe ni rahisi sana, kama wimbo wa kivita. Tusimameni sote na tujiandae kwa wimbo huu.. |

86. **<u>SOUNDS; FURNITURE BEING MOVED.</u>**

| | | |
|---|---|---|
| 87. | **CIRO** | (BEGINS TO SING)<br><br>Sisi wasichana tunahaki ya kuchagua taaluma tunazopenda. |
| 88. | **BOYS** | Wasichana mna uhuru wa kuchagua taaluma mtakazo |
| 89. | **GIRLS** | Naweza kuwa mhandisi |
| 90. | **BOYS** | Unaweza kuwa mhandisi |
| 91. | **GIRLS** | Nataka kuwa rubani |
| 92. | **BOYS** | Unaweza kuwa rubani. |
| 93. | **GIRLS** | Naweza kufanya chchote ninachotaka |
| 94. | **BOYS** | Unaweza kufanya chochote |
| 95. | **GIRLS** | Ni chagua langu. |
| 96. | **BOYS** | Ni chaguo lako |
| 97. | **GIRLS** | Ni chagua langu |
| 98. | **BOYS** | Ni chagua lako. |
| 99. | **ALL** | Ni chagua letu …Chagua lako, moja mbili.. tatu.. nne… HURRAY! |
| 100. | **ALL** | CLAPPING. LAUGHTER |

**101. Outro**

102. **NARRATOR**

Umekuwa mwisho mzuri sana ambapo wavulana kwa wasichana wanasherehekea waliyojifunza kuhusu kuchagua taaluma.Yaliyojitokeza ni kwamba Msichana yuko huru kuchagua taaluma yoyote, ilmradi awe ameipenda na anaweza kuifanya Hii ndio makala yetu ya mwisho katika mfululizo wa mchezo huu wa Learning by Ear Noa bongo jenga maisha yako kuhusu haki za wasichana.Mchezo ulioandikwa na NJOKI MUHOHO.

Hata hivyo usikose kusikiliza vipindi vingine vya Learning By Ear Noa Bongo Jenga Maisha yako.Tunakusukuru kwa kutusikiliza na iwapo ungependa kusikiliza tena kipindi hiki au vingine , au hata kutuma maoni yako tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.